



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA  
*(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))*



Kumb.Na.L.10/7/AB/56

10/02/2025

TANGAZO LA NAFASI YA  
KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kuomba nafasi ya kazi iliyotajwa hapo chini,

**1. AFISA HABARI DARAJA LA II – NAFASI I**

**1.0 SIFA ZA MWOMBAJI**

- Mwombaji awe amchitimu Shahada ya kwanza/Stashahada ya juu ya Uandishi wa Habari kutoka kwenye chuo kinachotambulika na Serikali.

**1.1 MAJUKUMU YA KAZI**

- Kukusanya na kuandika habari.
- Kupiga picha.
- Kuandaa picha za maonyesho.
- Kuhifadhi picha na kuhudumia Maktaba na marejeo.
- Kuandaa picha na marejeo (posters)
- Kukusanya takwimu mbalimbali.
- Kuandaa majorida mbalimbali na vipeperushi.

**1.2 NGAZI YA MSHAHARA**

Atalipwa kulingana na viwango vya Mishahara ya Serikali.

**MASHARTI YA JUMLA**

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
- Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili;
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.

- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maclezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale walofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates, -Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI, - Computer Certificate, -Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)
- v. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) HAVITAKUBALIWA.
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
- vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- viii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **24 Februari, 2025**.
- ix. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Aidha maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Posta au Mkono katika masijala ya wazi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kupitia anuani ifuatayo-;  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA**  
**MWANGA,**  
**S.L.P. 176,**  
**MWANGA.**
- x. Maombi ya takayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA**.
- xi. Limetolewa na;



Zahara A. Msangi

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**YA MWANGA**